JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU NA UTAMADUNI

KATALOGI YA VITABU VYA KIADA, ZIADA, REJEA NA VYA KUJISOMEA

(Juni 2004)

Sekretarieti
Kamati ya Kutathmini Machapisho ya Kielimu (EMAC)
S. L. P. 9121
Dar es Salaam
Tanzania
Simu: 022 2116192

Educational Material Approval Committee (EMAC)
Ministry of Education and Culture (MOEC)
June 2004

KATALOGI YA VITABU VYA

KIADA
(COURSE BOOKS)

ZIADA
(SUPPLEMENTARY BOOKS)

REJEA
(REFERENCE BOOKS)

NA

VYA KUJISOMEA
(READERS)

UTANGULIZI

Kwa mujibu wa Waraka wa Elimu Namba 2 wa 1998, machapisho yote yanayotumika kwa ajili ya kufundishia na kujifunza katika shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu Tanzania Bara, hayana budi yapate ithibati ya Wizara ya Elimu na Utamaduni kupitia kamati maalum inayofanya kazi hiyo yaani *Educational Materials Approval Committee* (EMAC).

Shughuli ya kutathmini machapisho kwa mujibu wa Waraka huu ilianza rasmi mwezi Novemba 1999. Machapisho yaliyopewa ithibati mwaka huo, yalipewa barua maalum ya Wizara kwa vile vyeti vilichelewa kuchapishwa. Wachapishaji waliagizwa waandike Namba ya Kumbukumbu ya barua hizo kwenye kila **Ukurasa-Jina wa machapisho** yao ili kama taarifa kwa wanunuzi. Vyeti vya Ithibati vilianza kutolewa rasmi kwa machapisho yaliyoidhinishwa kuanzia Januari mwaka 2000. Hivyo, machapisho yote yaliyochapishwa kuanzia mwaka huo na kuendelea yanatakiwa kuwa na kivuli cha cheti halisi cha ithibati. Cheti hiki kinaweza kuwa cha **rangi** (coloured) au **nyeusi-nyeupe** (black-in-white) na kinawekwa kwenye Ukurasa-Jina wa chapisho husika.

Pamoja na hilo, Wizara imekuwa ikitoa orodha ya machapisho yote yaliyopata ithibati kila robo mwaka na kuyasambaza kwa wadau wa elimu katika halmashauri mbali mbali kama vile Maafisaelimu wa Wilaya, Wakaguzi wa Shule wa Wilaya na Asasi na Taasisi zisizo za Kiserkali. Kwa muda wote huo mafanikio makubwa yamepatikana na sasa vitabu vya aina mbalimbali vipo shuleni japokuwa si vya kutosheleza.

Hata hivyo, yapo matatizo kadhaa yaliyojitokeza. Miongoni mwa hayo ni matumizi mabaya ya orodha hizo yaliyokuwa yakifanywa na baadhi ya wadau wasio waaminifu. Kwa mfano, machapisho ya baadhi ya wachapishaji yalikuwa yakifutwafutwa na kuingizwa mengine. Aidha, baadhi ya wadau walikuwa wakifanya siri na kuwanyima wengine wasijue ni machapisho gani yanatakiwa kununuliwa. Matokeo yake ni kwamba, shule nyingi zilipelekewa machapisho yasiyo kidhi haja. Katalogi hii linatarajiwa kuondoa upungufu huu.

Aidha, baada ya Serikali kufanya uamuzi wa kupeleka fedha za ununuzi wa vitabu shuleni, imeonekana kuna haja ya kuwapa habari rasmi walimu, walimu wakuu na kamati zao za shule ambao ndio wanunuzi wa vitabu sasa. Shule nyingi ziko vijijini ambako, mazingira ya usafiri na mawasiliano ni magumu sana. Katalogi itakuwa ni bora zaidi kuliko orodha tu. Wizara italisambaza Katalogi hii shuleni, kwenye ofisi za elimu za Kata, Wilaya, Mikoa na Ukaguzi wa Wilaya na Kanda. Aidha, wachapishaji na wauzaji wa vitabu watapata nakala.

Ndani ya Katalogi hii, kila kampuni ya uchapishaji imeonyeshwa kikamilifu yaani jina kamili, anuani na namba za simu. Taarifa hizi zitawarahisishia kazi wadau wote wa biashara ya vitabu vya shule. Aidha, orodha ya vitabu vya kila kampuni vimeonyeshwa pamoja na taarifa zao kadhaa kama vile Jina la chapisho, Mwaka wa kuchapishwa, Mahali kilipochapishwa, Ukubwa, Bei na Punguzo la Bei. Na mwisho kila chapisho lina maelezo mafupi. Ni matarajio yangu kuwa wadau wote watafaidika na yaliyomo kwenye Katalogi hii.

Educational Material Approval Committee (EMAC)
Ministry of Education and Culture (MOEC)
June 2004

Kwa sababu Wizara ilifanya marekebisho ya mitaala ya shule na vyuo mwaka 1996, Katalogi hii haionyeshi vitabu vya kiada na ziada vilivyochapwa kabla ya mwaka huo. Ila vitabu vya rejea na vile vya kujisomea vimeonyeshwa kwa sababu hivi havina haja ya kuzingatia muhtasari. *Hata hivyo, ninawashauri wachapishaji wote wavifanyie marekebisho vitabu vyao vyote vya miaka ya nyuma ili vishabihiane na muhtasari unaotumika sasa shuleni na vyuoni***.**

Ninawakumbusha wadau wote kuwa Ofisi yangu ingependa kupokea maoni yenu yatakayotusaidia kuboresha Katalogi hii.

R. A. Mpama
AFISAELIMU KIONGOZI
WIZARA YA ELIMU NA UTAMADUNI

YALIYOMO

1.	Utangulizi	**ii**
2.	Barka Publishers Limited	**1**
3.	Ben & Company Limited	**5**
4.	Business Publications Limited	**18**
5.	E & D Limited	**19**
6.	Educational Books Publishers limited	**24**
7.	EMITEC (UK) Limited	**39**
8.	General Publications Limited Bookshops & Stationers	**40**
9.	Heko Publishers	**44**
10.	KAI Limited	**45**
11.	Macmillan Aidan Limited	**46**
12.	Mathews Bookstore & Stationers	**75**
13.	Mkuki na Nyota Publishers Limited	**77**
14.	MPB Enterprises Publishers and Agencies	**81**
15.	Mture Educational Publishers Limited	**83**
16.	National Housing and Building Research Agency	**90**
17.	National Printing Company Limited	**91**
18.	Newjag (T) Limited	**92**
19.	Oxford University Press (T) Limited	**93**
20.	Press and Publicity Centre Limited	**113**
21.	Printcare Limited	**115**
22.	Readit Limited	**116**
23.	Ruvu Publishers Limited	**117**
24.	Sasa Maendeleo Trust Fund	**120**
25.	Taaluma Publishers Company Limited	**121**
26.	Tanzania Educational Publishers Limited	**122**
27.	Tanzania Publishing House	**126**
28.	Tanzania Schools Equipment Centre	**129**
29.	The Jomo Kenyatta Foundation	**130**
30.	The Star Books Limited	**132**
31.	Ujuzi / EAEP Limited	**133**
32	Yars & Co. Limited	**136**